ISSN 0856 – 01001X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

***No. 8*** ***31st August, 2022***

# *SPECIAL BILL SUPPLEMENT*

*to the Special Gazette of the United Republic of Tanzania No. 36 Vol. 103 dated 31st August, 2022*
*Printed by the Government Printer, Dodoma by Order of Government*

## MUSWADA WA SHERIA YA BIMA YA AFYA KWA WOTE WA MWAKA 2022

### MPANGILIO WA VIFUNGU

*Kifungu* *Jina*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina na kuanza kutumika.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.
4. Malengo.

SEHEMU YA PILI
MFUMO WA BIMA YA AFYA KWA WOTE

5. Wajibu wa ushiriki katika mfumo wa bima ya afya.
6. Mfumo wa bima ya afya.
7. Udhibiti wa mfumo wa bima ya afya.

SEHEMU YA TATU
SKIMU ZA BIMA YA AFYA

8. Skimu ya bima ya afya ya umma.
9. Skimu ya bima ya afya binafsi.
10. Skimu maalum ya bima ya afya.
11. Zuio la kuendesha skimu ya bima ya afya.

12. Utunzaji wa rejesta.
13. Kufuta usajili wa skimu ya bima ya afya.

SEHEMU YA NNE
VITITA VYA MAFAO

14. Vitita vya mafao.
15. Kitita cha mafao ya msingi.
16. Kitita cha huduma za ziada.
17. Wigo wa upatikanaji wa huduma za afya.

SEHEMU YA TANO
UANACHAMA NA UCHANGIAJI KATIKA SKIMU YA BIMA YA AFYA

18. Uanachama.
19. Wanufaika.
20. Usajili wa wanachama katika skimu ya bima ya afya.
21. Viwango vya uchangiaji.
22. Utambuzi na upatikanaji wa huduma kwa watu wasio na uwezo.
23. Uwekaji wa amana.
24. Utambuzi wa uanachama.
25. Ukomo wa uanachama.

SEHEMU YA SITA
UDHIBITI UBORA

26. Viwango vya udhibiti wa ubora vya skimu ya bima ya afya.
27. Udhibiti wa ubora wa watoa huduma za afya.

SEHEMU YA SABA
MASHARTI MENGINEYO

28. Ukwasi na uendelevu wa bima ya afya.
29. Uwekezaji wa skimu za bima za afya.
30. Gharama za usimamizi na uendeshaji.
31. Malalamiko na usuluhishi wa migogoro.
32. Zuio la kupata baadhi ya huduma pasipo kuwa na bima ya afya.
33. Mamlaka ya kutunga kanuni.
34. Taarifa za uongo.
35. Utaratibu wa madai ya skimu ya bima ya afya.
36. Makosa ya jumla.
37. Makosa yatendwayo na taasisi.
38. Mkinzano na sheria nyingine.

SEHEMU YA NANE
KUFUTWA KWA SHERIA NA MASHARTI YA MPITO

39. Kufutwa kwa Sheria na masharti yanayoendelea.
40. Masharti ya mpito.

SEHEMU YA TISA
MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI

*(a) Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, Sura ya 395*

41. Ufafanuzi.
42. Marekebisho ya kifungu cha 2.
43. Marekebisho ya kifungu cha 3.
44. Marekebisho ya kifungu cha 11.
45. Kufutwa na kuandikwa upya kwa kifungu cha 16.
46. Kufutwa na kuandikwa upya kwa kifungu cha 40.
47. Kufutwa kwa vifungu vya 41 na 42.

*(b) Sheria ya Hifadhi ya Jamii, Sura ya 135*

48. Ufafanuzi.
49. Marekebisho ya kifungu cha 3.

*(c) Sheria ya Bima, Sura ya 394*

50. Ufafanuzi.
51. Marekebisho ya kifungu cha 6.
52. Marekebisho ya kifungu cha 123.
53. Marekebisho ya kifungu cha 124.

*(d) Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii, Sura ya 50*

54. Ufafanuzi.
55. Kufutwa kwa vifungu vya 41, 42 na 43.
56. Marekebisho ya kifungu cha 45.

*(e) Sheria ya Paspoti na Hati za Kusafiria, Sura ya 42*

57. Ufafanuzi.
58. Marekebisho ya kifungu cha 12.

*(f) Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438*

59. Ufafanuzi.
60. Marekebisho ya kifungu cha 22.

*(g) Sheria ya Mtoto, Sura ya 13*

61. Ufafanuzi.
62. Marekebisho ya kifungu cha 8.

*(h) Sheria ya Leseni za Biashara, Na. 25 ya 1972*

63. Ufafanuzi.
64. Marekebisho ya kifungu cha 13.

*(i) Sheria ya Usalama Barabarani, Sura ya 168*

65. Ufafanuzi.
66. Marekebisho ya kifungu cha 25.

*(j) Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sura ya 366*

67. Ufafanuzi.
68. Kuongezwa kwa Sehemu Ndogo E.

*(k) Sheria ya Vyuo Vikuu, Sura ya 346*

69. Ufafanuzi.
70. Marekebisho ya kifungu cha 52.

*(l) Sheria ya Usajili na Utambuzi wa Watu, Sura ya 36*

71. Ufafanuzi.
72. Marekebisho ya kifungu cha 9.

*(m) Sheria ya Udhibiti wa Hospitali Binafsi, Sura ya 151*

73. Ufafanuzi.
74. Marekebisho ya kifungu cha 7.

## TAARIFA

Muswada huu utakaowasilishwa Bungeni umechapishwa pamoja na madhumuni na sababu zake kwa ajili ya kutoa taarifa kwa umma.

Dodoma,
30 Agosti, 2022

**HUSSEIN A. KATTANGA,**
*Katibu wa Baraza la Mawaziri*

## MUSWADA
*wa*

**Sheria kwa ajili ya kuweka masharti kuhusiana na mfumo wa bima ya afya kwa wote, kuimarisha mfumo wa bima ya afya kupitia bima ya afya kwa wote, kuweka masharti ya kupanua wigo wa huduma mbalimbali za afya; na kuweka masharti mengine yanayohusiana na hayo.**

**IMETUNGWA** na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## SEHEMU YA KWANZA
### MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina na kuanza kutumika

**1.**-(1) Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ya Mwaka 2022 na itaanza kutumika kwa tarehe ambayo Waziri, kwa tangazo litakalochapishwa kwenye Gazeti la Serikali, atateua.

(2) Wakati wa utekelezaji wa masharti ya kifungu kidogo cha (1), Waziri anaweza kuteua tarehe tofauti ya kuanza kutumika kwa masharti ya Sehemu au vifugu vya Sheria hii kwa kadri atakavyoona inafaa.

Matumizi

**2**. Sheria hii itatumika Tanzania Bara.

Tafsiri

**3.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

Sura ya 197

"Benki" maana yake ni Benki Kuu ya Tanzania iliyoanzishwa kwa Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania;

"bima ya afya kwa wote" maana yake ni utaratibu ulioainishwa kwa mujibu wa Sheria hii unaolazimu kila mwananchi kuwa na bima ya afya;

"kitita cha huduma za ziada" maana yake ni kitita cha huduma za afya zaidi ya kitita cha mafao ya msingi kinachotolewa na skimu ya bima ya afya;

"kitita cha mafao" maana yake ni huduma za afya zinazotolewa kwa mnufaika wa skimu ya bima ya afya;

"kitita maalum cha mafao" maana yake ni kitita cha mafao kitakachoanzishwa chini ya kifungu cha 8(2);

"kitita cha mafao ya msingi" maana yake ni kitita kinachotolewa na skimu za bima ya afya kwa wanufaika kwa uwiano, na inajumuisha kiwango cha uchangiaji;

"kituo cha huduma za afya" inajumuisha kliniki, zahanati, kituo cha afya, hospitali, maabara, duka la dawa au kituo kingine chochote kinachotoa huduma za afya;

"kituo cha huduma za afya kilichoingia mkataba" maana yake kituo cha kutolea huduma za afya kilichoingia makubaliano na skimu kuwahudumia wanufaika kwa mujibu wa Sheria hii;

"kiwango cha mchango" maana yake ni kiwango kutoka katika mshahara au chanzo kingine chochote kitakacholipwa katika skimu ya bima ya afya na mwanachama au kwa niaba ya mwanachama;

"kiwango cha uchangiaji" maana yake ni kiasi cha fedha kinacholipwa kwa lengo la kuwa mwanachama kwa mujibu wa Sheria hii;

Sura ya 394

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania iliyoanzishwa kwa Sheria ya Bima;

Sura ya 54

"mkazi" ina maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Uhamiaji;

"mnufaika" maana yake ni mtu anayestahili kupata mafao ya matibabu chini ya Sheria hii;

"mshahara" kwa madhumuni ya:

(a) mtumishi wa umma, maana yake ni mshahara usiojumuisha malipo ya ziada, stahiki, na posho;

(b) mwajiriwa wa sekta binafsi, maana yake ni mshahara unaojumuisha stahiki zote za kisheria zinazolipwa kama sehemu ya mshahara wa mwajiriwa;

"mtegemezi" maana yake ni-

(a) mzazi wa mwanachama au mzazi wa mwenza wa mwanachama;

(b) mtoto wa mwanachama wa kuzaa, kuasili au wa kambo aliye na umri chini ya miaka ishirini na moja; au

(c) ndugu wa damu wa mwanachama aliye na umri wa chini ya miaka ishirini na moja;

"mtoa huduma" inajumuisha kituo cha kutolea huduma za afya na skimu ya bima ya afya chini ya Sheria hii.

"mtu aliyejiajiri" maana yake ni mtu anayefanya kazi asiye katika uhusiano wa mwajiri na mwajiriwa;

"mtu asiye na uwezo" maana yake ni mtu ambaye ametambuliwa hivyo kwa mujibu wa kifungu cha 22;

Sura ya 366 "mwajiri" ina maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini;

Sura ya 366 "mwajiriwa" ina maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini;

"mwanachama" maana yake ni mtu yeyote aliyesajiliwa katika skimu chini ya Sheria hii na anachangia ama yeye mwenyewe au kupitia kwa Serikali;

Sura ya 357 "raia" ina maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Uraia;

"sekta isiyo rasmi" maana yake ni sekta inayojumuisha wafanyakazi wanaofanya kazi zisizo rasmi na ambao hawana mikataba ya ajira au mikataba mingine yoyote iliyoelezewa katika tafsiri ya neno "mwajiriwa" na inajumuisha mtu asiyejihusisha na aina yoyote ya uzalishaji;

"sekta rasmi" maana yake ni sekta inayojumuisha kazi zilizorasimishwa na kufanywa kwa mikataba ambapo mikataba hiyo imeainisha mishahara au ujira na muda maalum wa kazi;

"sekta rasmi binafsi" inajumuisha wafanyakazi katika mashirika au taasisi isipokuwa watumishi wa sekta ya umma;

"sekta ya umma" maana yake ni sekta inayojumuisha watumishi wa umma pamoja na wafanyakazi katika mashirika au taasisi binafsi ambayo Serikali inamiliki angalau asilimia thelathini ya hisa;

"skimu ya bima ya afya" maana yake ni bima ya afya ya umma au binafsi au bima maalumu iliyotambuliwa chini ya Sheria hii;

"skimu maalum ya bima ya afya" maana yake ni skimu itakayoanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 10(1) cha Sheria hii;

"skimu ya bima ya afya binafsi" maana yake ni bima ya afya iliyoanzishwa au kutambuliwa chini ya Sheria hii;

"skimu ya bima ya afya ya umma" maana yake ni bima ya afya iliyoanzishwa au kutambuliwa chini ya Sheria hii;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya masuala ya afya; na

"Wizara" maana yake ni Wizara yenye dhamana ya masuala ya afya.

Malengo

**4**. Malengo ya Sheria hii yatakuwa-
(a) kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za afya kwa wote kupitia mfumo wa bima ya afya;
(b) kuweka mfumo wa ushiriki katika skimu za bima ya afya kwa raia na wakazi wote.

## SEHEMU YA PILI
## MFUMO WA BIMA YA AFYA KWA WOTE

Wajibu wa ushiriki katika mfumo wa bima ya afya

**5**. Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, kila mtu anapaswa kujiunga na mfumo wa bima ya afya ili kuhakikisha anapata huduma za afya bila kikwazo cha fedha pindi anapozihitaji.

Mfumo wa bima ya afya

**6.** Mfumo wa bima ya afya kwa wote utajumuisha -
(a) waajiri na waajiriwa katika sekta ya umma na sekta rasmi binafsi;
(b) watu walioko katika sekta isiyo rasmi;
(c) skimu za bima ya afya;
(d) watu wasio na uwezo;
(e) vituo vya kutolea huduma za afya; na
(f) Mamlaka.

Udhibiti wa mfumo wa bima ya afya

**7**.-(1) Mamlaka ya Udhibiti wa bima iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Bima itakuwa ndiyo mamlaka ya udhibiti wa huduma za bima ya afya.

(2) Kwa madhumuni ya kuhakikisha ufanisi wa utekelezaji wa mfumo wa bima ya afya kwa wote, Mamlaka itakuwa na wajibu wa-
(a) kusajili skimu za bima ya afya;
(b) kufuatilia ubora wa huduma za afya zinazotolewa na vituo vya huduma za afya;
(c) kuhakikisha bima za afya zinatoa kitita cha mafao ya msingi kwa mujibu wa Sheria hii;

(d) kuhakikisha huduma za bima zinazotolewa zinaendana na viwango vya michango;
(e) kutoa miongozo ya malipo kwa watoa huduma;
(f) kutoa miongozo ya uendeshaji wenye ufanisi na tija katika usimamizi wa skimu za bima ya afya;
(g) kuhakikisha kuwa skimu ya bima ya afya ina ukwasi na akiba kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa;
(h) kutunza kanzidata ya vituo vya kutolea huduma za afya vilivyoingia mikataba na skimu za bima ya afya;
(i) kufanya ukaguzi wa skimu za bima ya afya;
(j) kuweka miongozo kuhusu usajili wa wanachama katika skimu za bima ya afya;
(k) kuomba au kuitisha taarifa yoyote itakayoihitaji; na
(l) kutekeleza jukumu lingine lolote kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa Sheria hii.

## SEHEMU YA TATU
### SKIMU ZA BIMA YA AFYA

Skimu ya bima ya afya ya umma
Sura ya 395

**8**.-(1) Kwa madhumuni ya Sheria hii, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulioanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya utatambulika kama skimu ya bima ya afya ya umma.

(2) Waziri kwa kushauriana na Mamlaka na kwa kuzingatia utaratibu utakaoainishwa katika kanuni, anaweza kuboresha skimu ya bima ya afya ya umma ikiwemo kuanzisha kitita maalum cha mafao kulingana na uhitaji kwa lengo la kufikia bima ya afya kwa wote.

Skimu ya bima ya afya binafsi

**9.**-(1) Mtu atakuwa na sifa ya kusajiliwa kuwa skimu ya bima ya afya ya binafsi baada ya kutimiza masharti kama yatakavyoainishwa katika kanuni chini ya Sheria hii.

Sura ya 394

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), kampuni au chombo kilichoidhinishwa chini ya Sheria ya Bima kutoa bima ya afya, kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, kitaendelea kutoa huduma kama skimu ya bima ya afya binafsi baada ya kutimiza masharti ya Sheria hii.

Skimu maalum ya bima ya afya

**10.**-(1) Mtu anayetoa mafao ya matibabu kwa waajiriwa wake katika namna yoyote mbali na utaratibu wa skimu za bima

ya afya ya umma na binafsi ulioainishwa kwa mujibu wa Sheria hii ataendela kutoa mafao hayo ya matibabu kwa waajiriwa wake:

Isipokuwa kwamba, mtu huyo atasajili mafao hayo kama skimu ya bima ya afya maalum kwa namna na jinsi ambavyo itaainishwa katika kanuni.

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), Mamlaka haitasajili mpango kama skimu maalumu iwapo mpango huo unahusisha sekta ya umma.

(3) Mtu ambaye, baada ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, anakusudia kutoa huduma za bima ya afya maalumu atapaswa kuwasilisha mpango wake katika Mamlaka kwa ajili ya kusajiliwa kwa namna na utaratibu utakaoainishwa katika kanuni.

Zuio la kuendesha skimu ya bima ya afya

**11**.-(1) Isipokuwa kama imeelezwa vinginevyo katika Sheria hii, mtu hataendesha skimu ya bima ya afya isipokuwa kama amepewa cheti cha usajili na Mamlaka kwa mujibu wa Sheria hii.

(2) Kila skimu ya bima ya afya itatatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia masharti kama yalivyoainishwa katika Sheria hii.

Utunzaji wa rejesta

**12**. Mamlaka itatunza rejesta ya skimu za bima ya afya zilizosajiliwa kwa mujibu wa Sheria hii na skimu nyingine za bima ya afya zilizokuwepo kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii.

Kufuta usajili wa skimu

**13**.-(1) Mamlaka inaweza kufuta usajili wa skimu ya bima ya afya iwapo-

(a) Sheria iliyoanzisha skimu ya bima ya afya ya umma imefutwa;
(b) skimu ya bima ya afya imekiuka masharti ya Sheria hii, kanuni au miongozo chini ya Sheria hii;
(c) skimu ya bima ya afya imesitisha kutoa huduma za bima au imefilisika;
(d) skimu ya bima ya afya imeomba kufutiwa usajili na Mamlaka imeridhia maombi hayo; au
(e) skimu ya bima ya afya imepoteza sifa za kusajiliwa kwa mujibu wa Sheria hii.

(2) Mamlaka, kabla ya kufuta usajili wa skimu ya bima ya afya, itatoa notisi ya angalau siku tisini ya kusudio lake la kufanya hivyo ikiitaka skimu ya bima ya afya kutoa sababu kwanini Mamlaka isifute usajili wa skimu hiyo.

(3) Mamlaka, kwa namna itakavyoainishwa katika kanuni, itaweka utaratibu utakaohakikisha kuwa wanachama hawaathiriki na kufutwa kwa skimu.

## SEHEMU YA NNE
## VITITA VYA MAFAO

Vitita vya mafao

**14**.-(1) Mwanachama au mnufaika wa skimu ya bima ya afya atakuwa na haki ya kupata kitita cha mafao ya msingi, kama hitaji la msingi, kama ambavyo itaainishwa chini ya Sheria hii.

(2) Kitita cha mafao ya msingi kitatumika kwa kipindi cha mwaka mmoja tangu tarehe ambayo mwanachama atasajiliwa kujiunga na Bima ya Afya:

Isipokuwa kwamba, kitita cha mafao ya msingi kwa mwanachama anayechangia kwa mujibu wa kifungu cha 21(1) na (2) kitaendelea kutumika hadi kufikia ukomo wake kwa kuzingatia masharti ya kifungu 25(2) cha Sheria hii.

(2) Bila kuathiri kifungu kidogo cha (1), mwanachama au mnufaika wa skimu ya bima ya afya, anaweza, kwa kutegemea mpango wa skimu husika, kupata kitita cha huduma za ziada.

(3) Skimu ya bima ya afya itatoa kitita cha mafao kwa mujibu wa kanuni zitakazotungwa chini ya Sheria hii.

Kitita cha mafao ya msingi

**15**.-(1) Waziri, kwa notisi itakayochapishwa katika Gazeti la Serikali, ataainisha kitita cha mafao ya msingi kitakachotolewa na skimu ya bima ya afya:

Isipokuwa kwamba, mabadiliko ya kitita cha mafao ya msingi yatazingatia matokeo ya tathmini ya uhai na uendelevu wa skimu za bima ya afya.

(2) Kila skimu ya bima ya afya, itatoa kitita cha mafao ya msingi kwa wanachama na wanufaika wake kama hitaji la msingi.

(3) Waziri, baada ya kushauriwa na Mamlaka, atafanya mapitio ya kitita cha mafao ya msingi katika vipindi mbalimbali kwa kadiri itakavyohitajika.

Kitita cha huduma za ziada

**16**.-(1) Skimu ya bima ya afya inaweza kutoa huduma ya ziada ya kitita cha mafao ya msingi kwa wanufaika wake; na michango kuhusiana na kitita cha huduma za ziada itakuwa kwa kuzingatia miongozo itakayotolewa na Mamlaka.

(2) Mamlaka itasimamia ushindani katika utoaji wa vitita vya huduma za ziada wa skimu za bima ya afya kwa madhumuni ya kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora.

Wigo wa upatikanaji wa huduma za afya

**17**. Mwanachama au mnufaika anaweza kupata huduma za afya mahala popote katika kituo cha kutolea huduma za afya kilichoingia mkataba na skimu ya bima ya afya kwa ajili ya utoaji wa huduma za afya.

## SEHEMU YA TANO
## UANACHAMA NA UCHANGIAJI KATIKA SKIMU YA BIMA YA AFYA

Uanachama

**18**.-(1) Uanachama katika skimu ya bima za afya utajumuisha watu wafuatao:

(a) watu wote ambao kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii walikuwa wanachama wa skimu ya bima ya afya kama ilivyoainishwa katika Sheria zinazosimamia skimu husika;
(b) watu wote ambao katika tarehe ya kuanza kutumika kwa Sheria hii watakuwa wametimiza umri wa miaka ishirini na moja;
(c) watu wote ambao, kwa tarehe ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, watakuwa chini ya umri wa miaka ishirini na moja lakini wanasifa za kusajiliwa kuwa wanachama kwa mujibu wa Sheria hii au Sheria nyingine yoyote;
(d) watu wote walioajiriwa katika sekta binafsi au ya umma;
(e) watu wote waliojiajiri;
(f) watu wasio na uwezo; na
(g) makundi mengine ya watu kadri itakavyoainishwa na Waziri katika kanuni.

(2) Mtu kutoka sekta rasmi binafsi au sekta isiyo rasmi atajiunga na skimu ya bima ya afya yoyote.

Wanufaika

**19**. Mwanachama anaweza kusajili watu wafuatao kama wanufaika:

(a) mwenza wa mwanachama; na
(b) wategemezi wasiozidi wanne.

Usajili wa wanachama katika skimu ya bima ya afya

**20**.-(1) Kwa kuzingatia utaratibu utakaoainishwa katika kanuni, mwajiri katika sekta ya umma na sekta rasmi binafsi atapaswa kumsajili mwajiriwa katika skimu ya bima ya afya ndani ya siku thelathini kutoka tarehe ya kuanza kwa mkataba wa ajira.

(2) Kila raia au mkazi aliye katika sekta rasmi na isiyo rasmi atasajiliwa katika skimu ya bima ya afya kwa utaratibu utakaoanishwa katika kanuni.

Viwango vya uchangiaji

**21**.-(1) Kwa madhumuni ya upatikanaji wa kitita cha mafao ya msingi, kila mwajiri chini ya sekta ya umma na sekta rasmi binafsi atawasilisha katika skimu asilimia sita ya mshahara wa mwajiriwa, ambapo ndani yake mwajiri atachangia nusu au zaidi ya kiwango hicho, na kiwango kilichosalia kitachangiwa na mwajiriwa.

(2) Waziri kwa kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha, ataainisha viwango vya uchangiaji kwa ajili ya sekta isiyo rasmi, kama itakavyoainishwa katika kanuni, kwa kuzingatia tathmini ya uhai na uendelevu wa skimu za bima ya afya katika utoaji wa kitita cha mafao ya msingi.

Utambuzi na upatikanaji wa huduma kwa watu wasio na uwezo

**22**.-(1) Waziri, kwa kushirikiana na mamlaka zinazohusika, na kwa kupitia kanuni, ataweka utaratibu na namna ya utambuzi wa watu wasio na uwezo.

(2) Watu watakaotambuliwa kama watu wasio na uwezo chini ya kifungu kidogo cha (1) watakuwa na haki ya kujumuishwa chini ya skimu ya bima ya afya kwa namna itakayoainishwa kwenye kanuni.

(3) Kwa madhumuni ya utekelezaji wa kifungu kidogo cha (2), Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha, kwa kushauriana na Waziri, ataainisha vyanzo mahususi kwa ajili ya ugharamiaji wa huduma za bima ya afya kwa watu wasio na uwezo.

(4) Waziri, kwa madhumuni ya Sheria hii, atatunza na kuhuisha kanzidata ya watu waliotambuliwa chini ya kifungu kidogo cha (1).

Uwekaji wa amana

**23**.-(1) Mtu anayeendesha skimu ya bima ya afya binafsi, kama sharti la usajili, ataweka Benki kiwango cha fedha kilichoainishwa kwenye kanuni kama amana ya huduma kwa wanachama.

(2) Skimu ya bima ya afya itatunza akiba ya kiasi cha fedha kitakachotosheleza utolewaji wa huduma kwa wanachama wake kwa kipindi cha angalau miaka miwili, kwa namna itakavyoainishwa katika kanuni.

(3) Amana inayorejewa katika kifungu kidogo cha (1) itadumu kwa kipindi chote cha uendeshaji wa skimu ya bima ya afya binafsi.

Utambuzi wa uanachama

**24**. Skimu ya bima ya afya itaweka utaratibu kwa ajili ya-
(a) upatikanaji wa utambulisho kwa mwanachama na wanufaika wake; na
(b) uhakiki wa utambulisho uliotolewa na huduma zinazotolewa na kituo cha kutolea huduma za afya.

Ukomo wa uanachama

**25**.-(1) Uanachama katika skimu ya bima ya afya utakoma baada ya kutokea kwa kifo cha mwanachama au pale ambapo mwanachama ataacha kuchangia kwenye skimu ya bima ya afya kwa kipindi kitakachoainishwa kwenye kanuni.

(2) Iwapo mwanachama anayechangia kupitia makato ya mshahara wake atafariki, wategemezi wake wataendelea kunufaika na huduma kwa kipindi kitakachoinishwa katika kanuni.

(3) Iwapo mwanachama anachangia kwa utaratibu wa michango kwa mwaka atafariki, wategemezi wake wataendelea kunufaika na huduma kwa kipindi kilichosalia cha mkataba wa uanachama.

## SEHEMU YA SITA
### UDHIBITI UBORA

Viwango vya udhibiti ubora vya skimu

**26.** Skimu ya bima ya afya itatekeleza viwango vya ubora vitakavyoainishwa na Mamlaka.

Udhibiti ubora wa watoa huduma za afya

**27**. Mamlaka itakuwa na jukumu la kuhakikisha kuwa vituo vya kutolea huduma vilivyoingia mikataba na skimu za bima ya afya vinatekeleza viwango vya ubora vilivyotolewa na Wizara au kwa mujibu wa Sheria.

## SEHEMU YA SABA
### MASHARTI MENGINEYO

Ukwasi na uendelevu wa bima ya afya

**28**.-(1) Skimu ya bima ya afya itatakiwa kufanya tathmini ya uhai na uendelevu kila baada ya miaka mitatu au wakati wowote kadiri itakavyokuwa imeelekezwa na Mamlaka kwa kumtumia mtathmini.

(2) Taarifa ya tathmini itakayofanywa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) itawasilishwa kwa Mamlaka na nakala kupelekwa kwa Waziri.

(3) Mamlaka inaweza kuelekeza skimu ya bima ya afya kuchukua hatua kama itakavyohitajika kurekebisha upungufu ulioonekana katika taarifa ya tathmini ya uhai na uendelevu.

Uwekezaji wa skimu ya bima ya afya

**29**.-(1) Uwekezaji wa skimu za bima ya afya za umma utazingatia miongozo itakayotolewa na Benki kwa kushauriana na Mamlaka.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1), Benki, kwa kushirikiana na Mamlaka, itakuwa na mamlaka ya-

(a) kutoa miongozo ya uwekezaji wa skimu za bima ya afya;
(b) kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa skimu za bima ya afya kwa wahusika wote chini ya Sheria hii; au
(c) kuchunguza na kukagua masuala yote yanayohusiana na usimamizi wa fedha wa skimu za bima ya afya.

Gharama za usimamizi na uendeshaji

**30**. Mamlaka itatoa miongozo kuhusu ukomo wa juu wa gharama za uendeshaji wa skimu ya bima ya afya ya umma.

Malalamiko na usuluhishi wa migogoro
Sura ya 394

**31**. Utaratibu wa kushughulikia malalamiko na utatuzi wa migogoro baina ya au dhidi ya skimu ya bima ya afya, kituo cha huduma za afya kilichoingia mkataba, mnufaika, mwajiri na mtu yeyote anayehusika utakua kama ulivyoainishwa kwenye Sheria ya Bima.

Zuio la kupata baadhi ya huduma pasipo kuwa na bima ya afya

**32**. Kwa kuzingatia sheria zilizotungwa na Bunge, mamlaka zinazohusika na usimamizi au utoaji wa -

(a) leseni ya udereva;
(b) bima za vyombo vya moto;
(c) utambulisho wa mlipa kodi;
(d) usajili wa laini za simu;
(e) leseni ya biashara au
(f) hati ya kusafiria au viza;
(g) uandikishaji wa wanafunzi wa kidato cha tano, kidato cha sita na vyuoni; na
(h) utoaji wa kitambulisho cha Taifa,

zitahakikisha kuwa usajili au utoaji wa vibali, hati au leseni kwa waombaji unazingatia kigezo cha uwepo wa uthibitisho wa uanachama katika skimu ya bima ya afya.

Mamlaka ya kutunga kanuni

**33**. Waziri anaweza kutengeneza kanuni zitakazoainisha:
(a) utaratibu wa usajili wa skimu za bima ya afya;
(b) kitita cha mafao, muda, masharti au wigo wa kitita cha mafao kwa kushirikiana na Mamlaka;
(c) utaratibu wa kuanzisha kitita cha mafao maalum katika skimu ya bima ya afya ya umma;
(d) muda wa kuahirishwa kwa malipo yoyote ya madai wakati uchunguzi unaendelea;
(e) utaratibu wa kusajiliwa kwenye skimu ya bima ya afya kwa watu wenye umri chini ya miaka ishirini na moja;
(f) utaratibu wa ulipaji wa faini zote au sehemu ya faini kwa kuzingatia masharti kama yatakavyoainishwa;
(g) utaratibu wa utambuzi wa watu walio katika sekta isiyo rasmi na namna ya kuwasajilii katika skimu;
(h) maelezo, taarifa, uthibitisho au ushahidi utakaotolewa kwa suala lolote au jambo linalojitokeza chini ya Sheria hii, ikiwemo suala lolote au jambo muhimu kuhusiana na malipo ya michango aliyolipa mwanachama au kuhusiana na mtu yeyote au uandaaji au uhalalishaji wa madai yoyote au maombi kwa ajili ya malipo ya mafao yoyote yanayotolewa chini ya Sheria hii;
(i) utaratibu wa malipo kwa vituo vya kutolea huduma za afya;
(j) hatua yoyote inayohitajika au kuruhusiwa kuchukuliwa chini ya Sheria hii, muda na namna ya kuchukua hatua hiyo, utaratibu utakaofuatwa na fomu zitakazotumika;
(k) utambuzi na usajili wa watu wasio na uwezo kwa kushirikiana na mamlaka nyingine;
(l) namna ya upatikanaji wa huduma za afya kwa watu wasio na uwezo;
(m) utaratibu wa kuboresha kitita cha mafao katika skimu ya bima ya afya ya umma; na
(n) suala lingine lolote kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

Taarifa za uongo

**34**. Mtu yeyote ambaye-
(a) anatoa taarifa za uongo;
(b) anashindwa kuwasilisha nyaraka zinazohitajika chini ya Sheria hii pasipo kuwa na sababu za msingi,

anatenda kosa na akitiwa hatiani, atawajibika -

(i) kwa kosa lililotendwa na mwanachama au mnufaika, kulipa faini isiyopungua shilingi laki

mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi kumi na mbili au vyote;

(ii) kwa kosa lililotendwa na skimu ya bima ya afya au kituo cha kutolea huduma za afya kilichoingia mkataba, kulipa faini isiyopungua shilingi milioni tano na isiyozidi shilingi milioni mia moja.

Utaratibu wa madai ya skimu ya bima ya afya

**35**.-(1) Mahakama inayosikiliza shauri dhidi ya mtu yoyote aliyeshtakiwa kwa kosa chini ya Sheria hii, bila kujali uwepo wa shauri lolote la madai, inaweza kuamuru mshtakiwa kuilipa skimu ya bima ya afya kiasi cha mchango kinachodaiwa pamoja na faini itakayotozwa au gharama nyingine yeyote, na kiasi kitakachoamriwa kinaweza kudaiwa na kulipwa kwa skimu.

(2) Kiasi chochote kinachodaiwa na skimu ya bima ya afya kitakuwa ni deni kwa skimu na, bila kuathiri namna nyingine ya kudai, kiasi hicho kinaweza kudaiwa kwa njia ya madai ya haraka kwa mujibu wa kanuni ya XXXV ya Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai.

Sura ya 33

Makosa ya jumla

**36**. Mtu anayekiuka masharti yoyote ya Sheria hii anatenda kosa na pale ambapo hakuna adhabu mahsusi iliyowekwa, mtu huyo, akitiwa hatiani, atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi milioni hamsini au kutumikia kifungo kisichopungua mwaka mmoja au vyote.

Makosa yatendwayo na taasisi

**37.** Endapo kosa limetendwa na kampuni au taasisi chini ya Sheria hii, mkurugenzi, meneja au mbia wa kampuni au taasisi hiyo atawajibika, ikiwa atatiwa hatiani, kwa adhabu iliyoainishwa kuhusiana na kosa hilo, isipokuwa kama mkurugenzi, meneja au mbia huyo ataithibitishia mahakama kwa kiasi cha kuiridhisha kwamba kitendo kilichosababisha kosa hilo kufanyika kilifanyika pasipo yeye kuwa na uelewa, kutoa idhini au kuchukua hatua za makusudi kuzuia kosa hilo kutendeka.

Mkinzano na sheria nyingine

**38**. Endapo kutakuwa na mkinzano baina ya masharti ya Sheria hii na masharti ya sheria nyingine yoyote kuhusiana na masuala ya bima ya afya, masharti ya Sheria hii yatapewa kipaumbele.

## SEHEMU YA NANE
### KUFUTWA KWA SHERIA NA MASHARTI YA MPITO

**39**.-(1) Sheria ya Mfuko wa Afya ya Jamii inafutwa.

Kufutwa kwa Sheria na masharti yanayoendelea
Sura ya 409

(2) Bila kujali kufutwa kwa Sheria chini ya kifungu kidogo cha (1)-

(a) kanuni, amri, miongozo na sheria ndogo nyingine zilizotungwa chini ya Sheria ya Mfuko wa Afya ya Jamii na ambazo zilikuwa zinatumika kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, zitaendelea kutumika hadi zitakapofutwa;

(b) maelekezo yote yaliyotolewa chini ya masharti ya Sheria ya Mfuko wa Afya ya Jamii yataendelea kuwa halali hadi hapo yatakapofutwa, kusitishwa au kukoma kutokana na sababu ya kuisha kwa muda wake;

(c) mtu ambaye wakati wa kuanza kutumika kwa Sheria hii alikuwa akinufaika na mafao ya Mfuko wa Afya ya Jamii ataendelea kunufaika na mafao hayo hadi muda wa uanachama wake utakapokoma; na

(d) haki na afua ambazo, kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii zilitolewa kwa mujibu wa Sheria ya Mfuko wa Afya ya Jamii, zitaendelea kuwepo kana kwamba zilitolewa chini ya Sheria hii hadi hapo zitakapofutwa kwa mujibu wa Sheria hii.

Masharti ya mpito

**40**.-(1) Kutakuwa na kipindi cha mpito kisichozidi miezi kumi na mbili, kitakachoanzia tarehe ya kuanza kutumika kwa Sheria hii.

(2) Kwa kuzingatia Sheria hii na kabla kuisha kwa kipindi cha mpito, Wizara kwa kushirikiana na Wizara yenye dhamana na mamlaka za serikali za mitaa na mamlaka nyingine husika, itaratibu uhitimishwaji wa shughuli za Mfuko wa Afya ya Jamii ikiwa ni pamoja na utambuzi wa mali, madeni, madai, hatma ya mikataba iliyopo, mashauri yaliyopo na masuala mengine yanayohusiana na Mfuko wa Afya ya Jamii kwa namna itakavyoainishwa katika kanuni.

(3) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), Waziri anaweza kuongeza muda wa kipindi cha mpito kwa kipindi kingine cha ziada kisichozidi miezi sita.

## SEHEMU YA TISA
### MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI

*(a) Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, Sura ya 395*

Ufafanuzi
Sura ya 395

**41.** Sehemu Ndogo hii itasomwa pamoja na Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ambayo hapa itarejewa kama "Sheria Kuu".

Marekebisho ya kifungu cha 2

**42.** Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 2(1) kwa kuongeza maneno "persons under formal private sector, students" kati ya maneno "Councillors," na "retirees".

Marekebisho ya kifungu cha 3

**43.** Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 3 kwa kufuta tafsiri ya neno "Authority" na badala yake kuweka tafsiri ifuatayo:

" "Authority" has the meaning ascribed to it under the Universal Health Insurance Act;".

Marekebisho ya kifungu cha 11

**44.** Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu 11(1) kwa kuongeza maneno "persons under formal private sector, student and children" baada ya neno "Councilors" lililopo katika aya (e).

kufutwa na kuandikwa upya kwa kifungu cha 16

**45**. Sheria Kuu inarekebishwa kwa kufuta kifungu cha 16 na badala yake kuweka kifungu kifuatacho:

"Benefit package

**16.-** (1) The Fund shall provide the standard benefit package in accordance with the Universal Health Insurance Act.

(2) Without prejudice the provisions of subsection (1), the Fund may provide supplementary benefit packages in accordance with the Universal Health Insurance Act.".

Kufutwa na kuandikwa upya kwa kifungu cha 40

**46**. Sheria Kuu inarekebishwa kwa kufuta kifungu cha 40 na badala yake kuweka kifungu kifuatacho:

"Appeal

**40**. A member or health care provider who is aggrieved by any decision of an officer of a scheme may appeal to the Ombudsman through the Authority in accordance with section 124(5) of the Insurance Act.".

Cap. 394

Kufutwa kwa vifungu vya 41 na 42

**47**. Sheria ya Kuu inarekebishwa kwa kufuta vifungu vya 41 na 42.

*(b) Sheria ya Hifadhi ya Jamii, Sura ya 135*

Ufafanuzi
Sura ya 135

**48**. Sehemu Ndogo hii itasomwa pamoja na Sheria ya Hifadhi ya Jamii ambayo hapa itarejewa kama "Sheria Kuu".

Marekebisho ya kifungu cha 3

**49**. Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 3 katika tafsiri ya neno "social security scheme" kwa kuondoa maneno "health care needs".

*(c) Sheria ya Bima, Sura ya 394*

Ufafanuzi
Sura ya 394

**50**. Sehemu Ndogo hii itasomwa pamoja na Sheria ya Bima ambayo hapa itarejewa kama "Sheria Kuu".

Marekebisho ya kifungu cha 6

**51**. Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 6-

(a) katika kifungu kidogo cha (1), kwa kuongeza maneno "health insurance scheme members, employers, health service providers and health insurance schemes" baada ya neno "policy-holders";

(b) katika kifungu kidogo cha (2) kwa-

(i) kuongeza maneno "health insurance scheme members, employers, health service providers and health insurance schemes" baada ya neno "policy-holder" lililopo mwishoni mwa aya (j);

(ii) kuongeza aya mpya mara baada ya aya (k) kama ifuatavyo:

"(l) oversee and ensure quality assurance of the primary benefit package and contribution rates in collaboration with the Ministry responsible for health matters;

(m) supervise and regulate funds, insurance companies and health care providers;

(n) supervise the compliance of laws related with insurance;" na

(iii) kubadilisha mpangalio wa aya (l) na (m) kuwa aya (o) na (p), mtawalia.

Marekebisho ya kifungu cha 123

**52. S**heria Kuu inarekebishwa kwa-

(a) kukifanya kifungu cha 123 kuwa kifungu cha 123(1); na

(b) kuongeza mara baada ya kifungu kidogo cha (1) kifungu kidogo cha (2) kama ifuatavyo:

"(2) Notwithstanding subsection (1)-

(a) health insurance schemes may file to the Ombudsman complaints against a member of a

health insurance scheme or a health service provider; and

(b) a member of a health insurance scheme and health service provider may file to the ombudsman applications for review against the decision of a health insurance scheme.".

Marekebisho ya kifungu cha 124

**53.** Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 124 kwa kuongeza mara baada ya kifungu kidogo cha (4), kifungu kidogo cha (5) kama ifuatavyo:

"(5) Notwithstanding subsection (1), the Ombudsman shall have unlimited jurisdiction to determine health insurance related complaints from a member of a health insurance scheme or a health service provider referred to it by the Authority."

*(d) Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii, Sura ya 50*

Ufafanuzi Sura ya 50

**54.** Sehemu Ndogo hii itasomwa pamoja na Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii, ambayo hapa itarejewa kama "Sheria Kuu".

Kufutwa kwa vifungu vya 41, 42, na 43

**55.** Sheria Kuu inarekebishwa kwa kufuta vifungu vya 41, 42 na 43.

Marekebisho ya kifungu cha 45

**56.** Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 45 kwa kuongeza maneno "granted in accordance with the Universal Health Insurance Act" baada ya neno "midwife" lililopo mwishoni mwa aya (b).

*(e) Sheria ya Paspoti na Hati za Kusafiria, Sura ya 42*

Ufafanuzi Sura ya 42

**57.** Sehemu Ndogo hii itasomwa pamoja na Sheria ya Paspoti na Hati za Kusafiria ambayo hapa itarejewa kama "Sheria Kuu".

Marekebisho ya kifungu cha 12

**58**. Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 12(2) kwa kuongeza mara baada ya aya (d) aya ifuatayo:

"(e) a proof of registration with a health insurance scheme.".

*(f) Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438*

Ufafanuzi
Sura ya 438

**59.** Sehemu Ndogo hii itasomwa pamoja na Sheria ya Usimamizi wa Kodi ambapo hapa itarejewa kama "Sheria Kuu".

Marekebisho ya kifungu cha 22

**60**. Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 22(4) kwa kuongeza maneno "and membership with a health insurance scheme" mara baada ya neno "identity" lililopo katika aya (b).

*(g) Sheria ya Mtoto, Sura ya 13*

Ufafanuzi
Sura ya 13

**61**. Sehemu Ndogo hii itasomwa pamoja na Sheria ya Mtoto ambayo hapa itarejewa kama "Sheria Kuu".

Marekebisho ya kifungu cha 8

**62.** Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 8 kwa kuongeza kifungu kidogo cha (7) kama ifuatavyo:

> "(7) For the purpose of ensuring attainment of the right of a child to medical care, a parent, guardian or any other person having custody of a child shall enroll the child with a health insurance scheme."

*(h) Sheria ya Leseni za Biashara, Na. 25 ya 1972*

Ufafanuzi
Sura ya 208

**63.** Sehemu Ndogo hii itasomwa pamoja na Sheria ya Leseni za Biashara ambayo hapa itarejewa kama "Sheria kuu".

Marekebisho ya kifungu cha 13

**64.** Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 13 kwa kuongeza mara baada ya neno "Authority" maneno ", proof of registration with a health insurance scheme by business owners and employees".

*(i) Sheria ya Usalama Barabarani, Sura ya 168*

Ufafanuzi
Sura ya 168

**65**. Sehemu Ndogo hii itasomwa pamoja na Sheria ya Usalama Barabarani ambapo hapa itarejewa kama "Sheria Kuu".

Marekebisho ya kifungu cha 25

**66.** Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 25-

(a) katika kifungu kidogo cha (1), kwa kuongeza maneno "proof of membership to health insurance scheme" baada ya maneno "prescribed fee"; na

(b) katika kifungu kidogo cha (2), kwa kuongeza maneno "proof of membership to health insurance scheme" baada ya maneno "prescribed fee".

*(j) Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sura ya 366*

Ufafanuzi Sura ya 366

**67.** Sehemu Ndogo hii itasomwa pamoja na Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ambapo hapa itarejewa kama "Sheria Kuu".

Kuongezwa kwa Sehemu Ndogo E

**68.** Sheria Kuu inarekebishwa kwa kuongeza mara baada ya kifungu cha 11 Sehemu Ndogo ya E kama ifuatavyo-

"*Sub-Part E- Access to health insurance*

Access to health insurance

**11A.-**(1) Subject to the provisions of the Universal Health Insurance Act, the employer shall register his employee with a health insurance scheme.

(2) A person who contravenes the provisons of this section commits an offence."

*(k) Sheria ya Vyuo Vikuu, Sura ya 346*

Ufafanuzi Sura 346

**69**. Sehemu Ndogo hii itasomwa pamoja na Sheria ya Vyuo Vikuu ambapo hapa itarejewa kama "Sheria Kuu".

Marekebisho ya kifungu cha 52

**70**. Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 52(2) kwa kuongeza maneno "and has submitted proof of registration with a health insurance scheme" mara baada ya maneno "subsection (1)".

*(l) Sheria ya Usajili na Utambuzi wa Watu, Sura ya 36*

Ufafanuzi Sura ya 36

**71**. Sehemu Ndogo hii itasomwa pamoja na Sheria ya Usajili na Utambuzi wa Watu ambapo hapa itarejewa kama "Sheria Kuu".

Marekebisho ya kifungu cha 9

**72**. Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 9(1)(b) kwa-

(a) kuongeza mara baada ya aya ndogo ya (vi), aya ndogo ifuatayo-

" (vii) proof of registration with a health insurance scheme;"; na

(b) kubadilisha mpangilio wa aya ndogo za (vii) na (viii) kuwa aya ndogo za (viii) na (ix) mtawalia.

*(m) Sheria ya Udhibiti wa Hospitali Binafsi, Sura ya 151*

Ufafanuzi Sura ya 151

**73**. Sehemu Ndogo hii itasomwa pamoja na Sheria ya Udhibiti wa Hospitali Binafsi ambapo hapa itarejewa kama "Sheria Kuu".

Marekebisho ya kifungu cha 7

**74**. Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 7(2)-

(a) kwa kuongeza mara baada ya aya (b), aya ifuatayo-

"(c) the Commissioner of Insurance or a person nominated on his behalf from the Tanzania Insurance Regulatory Authority;";

(b) kwa kubadilisha mpangilio wa aya (c) kuwa aya (d); na

(c) katika aya (d) kama ilivyobadilishwa, kwa kufuta neno "five" na badala yake kuweka neno "four".

## MADHUMUNI NA SABABU

Muswada huu unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ya Mwaka 2022 na kuweka mfumo wa usimamizi na udhibiti wa utoaji wa huduma za bima ya afya kwa wote. Kutungwa kwa Sheria hii kutawezesha raia na wakazi wote kuwa na uhakika wa kupata huduma za afya bila kikwazo cha fedha.

Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Kuu Tisa.

Sehemu ya Kwanza inahusu masharti ya awali ikijumuisha jina la Muswada, mawanda ya Sheria inayopendekezwa, tafsiri ya maneno mbalimbali kama yalivyotumika katika Sheria pamoja na malengo ya Muswada.

Sehemu ya Pili ya Muswada inaweka masharti kuhusiana na mfumo wa bima ya afya kwa wote. Katika kifungu cha 5 kinaweka wajibu wa kila mtu kujiunga na mfumo wa bima ya afya ambapo dhumuni la kifungu hicho ni kuhakikisha watu wote wanapata huduma za afya bila kikwazo cha fedha pindi wanapozihitaji. Kifungu cha 6 inapendekezwa kuanzisha mfumo wa bima ya afya kwa wote ambapo makundi mbalimbali yatajumuishwa na kushiriki kwa namna ambayo itahakikisha kuwa kila mtu anajiunga na skimu za bima ya afya. Kifungu cha 7 kinaweka masharti kuhusu namna Mamlaka ya Usimamizi wa Bima itakavyokuwa na jukumu la kudhibiti mfumo wa bima ya afya. Kwa mujibu wa kifungu hicho, Mamlaka itakuwa na wajibu wa kusajili na kudhibiti skimu za bima ya afya, kusimamia ubora wa huduma za afya zinazotolewa na vituo vya kutolea huduma za afya vyenye mikataba na skimu za bima ya afya, kuhakikisha kuwa kila skimu ya bima ya afya inatoa kitita cha mafao ya msingi kwa

mujibu wa Sheria hii, na kutoa miongozo kuhusiana na uendeshaji wenye tija na ufanisi wa shughugli za skimu za bima ya afya.

Sehemu ya Tatu ya Muswada inaweka masharti kuhusiana na skimu za bima ya afya. Kifungu cha 8 kinatambua Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kama skimu ya bima ya afya ya umma na kumpa Waziri mwenye dhamana na afya kwa kushirikiana na Mamlaka ya usimamizi wa bima nchini, jukumu la kuboresha skimu za bima ya afya ya umma. Dhumuni la kifungu hiki ni kuhakikisha uendelevu wa upatikanaji wa huduma kwa wanachama wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya na kuboresha skimu za bima ya afya ikiwa ni pamoja na kuanzisha kitita cha mafao maalum kulingana na uhitaji ili kuwajumuisha wananchi wote katika mfumo wa bima ya afya kwa wote. Kifungu cha 9 kinatoa nafasi kwa kampuni binafsi kusajiliwa kama skimu za bima ya afya binafsi baada ya kutimiza vigezo na masharti yatakayoainishwa chini ya kanuni zitakazotungwa chini ya Sheria inayopendekezwa. Dhumuni la kifungu hiki ni kutambua umuhimu wa bima za afya binafsi katika kukuza ushindani na kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma za bima ya afya nchini. Kifungu cha 10cha Sehemu hii kinatambua skimu maalum za bima ya afya ambazo ni tofauti na bima ya afya ya umma na binafsi. Skimu hizo ni zile ambazo makampuni binafsi yana utaratibu maalumu wa kuwapitia huduma za afya wafanyakazi wake. Dhumuni la kifungu hiki ni kuweka utaratibu wa kuhakikisha skimu hizo zinakidhi matakwa ya Sheria inayopendekezwa.

kifungu cha 11 cha sehemu hii kinaweka katazo la uendeshaji wa skimu za bima ya afya bila kusajiliwa. Dhumuni ni kuhakikisha kuwa skimu za bima ya afya zinajiendesha kwa mujibu wa Sheria inayopendekezwa. Vilevile, kifungu cha 12 kinaipa Mamlaka uwezo wa kutunza rejesta ya skimu za bima ya afya zilizosajiliwa chini ya Sheria hii, kwa lengo la kuhakikisha uratibu na usimamizi wa skimu hizo. Aidha, kifungu cha 13 kinaweka masharti kuhusu

sababu na utaratibu ambao Mamlaka itaufuata katika kufuta usajili wa skimu za bima ya afya na hatua zinazotakiwa kuchukuliwa iwapo skimu ya bima ya afya itataka kujiondoa katika utoaji wa huduma za bima ya afya. Dhumuni la kifungu hiki ni kuhakikisha huduma za bima ya afya zinazotolewa na skimu za bima ya afya zinakidhi vigezo.

Sehemu ya Nne ya Muswada inaweka masharti kuhusiana na vitita vya mafao. Kifungu cha 14 kinaweka masharti kuhusu utoaji wa kitita cha mafao ya msingi kwa wanufaika wa skimu za bima ya afya. Vilevile, kifungu hicho kinatoa fursa ya utoaji wa kitita cha mafao ya ziada kinachojumuisha huduma zilizo nje ya kitita cha mafao ya msingi. Lengo la kifungu hiki ni kuhakikisha kila mwananchi anapata huduma za kitita cha mafao ya msingi kwa uwiano, na kutoa fursa ya upatikanaji wa huduma za afya ambazo hazijajumuishwa katika kitita cha mafao ya msingi. Kifungu cha 15 kinampa Waziri mamlaka ya kuainisha kitita cha mafao ya msingi kitakachotolewa na skimu za bima za afya ambapo kila skimu itatakiwa kutoa kitita hicho kifungu hicho kinaweka muda kutumika kwa kitita cha mafao ya msingi. Dhumuni la kifungu hiki ni kuhakikisha skimu za bima ya afya zinazingatia utoaji wa kitita cha mafao ya msingi ambacho ni haki ya kila mnufaika.

Ili kuhakikisha skimu za bima ya afya zinatoa kitita cha mafao ya ziada kwa kuzingatia gharama halisi, kifungu cha 16 kinaweka masharti ya utoaji wa kitita cha mafao cha ziada kama itakavyoidhinishwa na Mamlaka. Kifungu cha 17 kinaainisha wigo wa upatikanaji wa huduma za afya kwa vituo vyote vya kutolea huduma za afya vilivyoingia mkataba na skimu za bima ya afya kwa lengo la kuhakikisha wanufaika wanafikiwa na huduma popote walipo.

Sehemu ya Tano ya Muswada inaweka masharti kuhusiana na uanachama na uchangiaji katika skimu za bima ya afya. Kifungu

cha 18 kinafafanua watu wanaopaswa kujiunga na skimu za bima ya afya na kuhimiza kila mtu kujiunga. Kifungu cha 19 kinaelezea aina na idadi ya watu wanaoweza kujumuishwa katika skimu za bima ya afya na mwanachama mchangiaji kama wanufaika wake. Vilevile, kifungu cha 20 kinaweka utaratibu kuhusiana na usajili wa wanachama ambapo waajiri katika sekta za umma na binafsi watatakiwa kuwasajili waajiriwa wao ndani ya siku 30 toka kuanza kwa mkataba wa ajira. Aidha, kila raia ama mkazi aliyeko katika sekta isiyo rasmi atatakiwa kujiunga na skimu ya bima ya afya chini ya Sheria inayopendekezwa. Kwa muktadha wa Sheria inayopendekezwa, sekta ya umma inajumuisha watumishi wa umma pamoja na wafanyakazi katika mashirika au taasisi binafsi ambayo Serikali ina miliki hisa kwa asilimia thelathini au zaidi kama inavyotekelezwa katika mifuko ya hifadhi ya jamii. Lengo ni kuwa na tafsiri ya pamoja kama inavyotafsiriwa na kutumika katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na kuwajumuisha waajiri na waajiriwa waliopo katika mashirika na taasisi ambazo Serikali ina hisa ili kuongeza uhimilivu wa Mifuko ya bima ya afya ya umma.

Kifungu cha 21 kinaainisha utaratibu wa uchangiaji katika skimu za bima ya afya kwa sekta ya umma, sekta rasmi binafsi na sekta isiyo rasmi. Mwajiri wa sekta ya umma na sekta rasmi binafsi atawasilisha katika bima ya afya asilimia sita ya mshahara wa mwajiriwa, ambapo mwajiri atachangia nusu au zaidi ya kiwango hicho na mwajiriwa atachangia kiwango kilichobaki. Katika sekta isiyo rasmi, kaya ya watu sita itachangia kiwango kitakachoainishwa na Waziri mwenye dhamana katika kanuni za Sheria inayopendekezwa. Kwa sekta ya umma na rasmi binafsi michango itatokana na mishahara inayolipwa kwa waajiriwa, hivyo kwa muktadha wa Sheria hii mshahara imetafsiriwa kwa maana sawa na inayotumika na Mifuko ya Pensheni. Dhumuni la kifungu hiki ni kuwa na maana zinazofanana na zinazotumika na Mifuko ya Pensheni inayosimamia sekta ya umma na sekta rasmi binafsi pamoja na kuhakikisha uwiano katika uchangiaji wa kitita

cha mafao ya msingi. Kifungu cha 22 kinaweka utaratibu wa utambuzi na usajili wa kundi la watu wasiokuwa na uwezo kwa lengo la kuhakikisha wanapata huduma za afya bila kikwazo cha fedha kwa utaratibu utakaowekwa na Sheria inayopendekezwa.

Katika kuhakikisha uendelevu wa upatikanaji wa huduma kwa wanufaika, kifungu cha 23 kinaweka sharti kwa skimu za bima ya afya kuweka na kutunza amana katika Benki Kuu ya Tanzania ambayo itatumika endapo skimu hizo zitashindwa kuendelea kutoa huduma kwa wanufaika wake kutokana na sababu mbalimbali. Vilevile, kifungu cha 24 kinaweka utaratibu wa utambuzi wa wanachama na wanufaika kwa lengo la kupata taarifa zitakazowezesha kuhakiki usahihi wa wanachama na kudhibiti udanganyifu. Pia, kifungu cha 25 kinaweka utaratibu kuhusu ukomo wa uanachama ambapo ukomo huo utafikiwa pale ambapo mwanachama amefariki au anaacha kuchangia katika skimu ya bima ya afya. Dhumuni la kifungu hiki ni kulinda haki za mnufaika pamoja na kulinda uhai na uendelevu wa skimu za bima ya afya.

Sehemu ya Sita ya Muswada inaweka masharti kuhusiana na udhibiti ubora wa huduma zitolewazo na vituo vya kutolea huduma za afya na skimu za bima ya afya. Kifungu cha 26 kina lengo la kuhakikisha skimu za bima ya afya zinazingatia ubora katika utoaji wa huduma za bima ya afya kulingana na miongozo ya Mamlaka. Kifungu cha 27 kinaipa Mamlaka jukumu la kuhakikisha vituo vya kutolea huduma za afya vilivyoingia mikataba na skimu za bima ya afya vinatoa huduma bora za afya kwa wanufaika.

Sehemu ya Saba inaweka masharti mengineyo ambayo kwa namna moja au nyingine yatahusika katika utekelezaji wa masharti ya Sheria inayopendekezwa. Uendeshaji wa skimu utazingatia kanuni za uendeshaji wa bima za afya. Kifungu cha 28 kinaweka masharti kwa kila skimu ya bima ya afya kufanya tathmini ya uhai na

uendelevu kila baada ya miaka mitatu au wakati wowote kadiri itakavyoelekezwa na Mamlaka. Kifungu cha 29 kinaipa Benki Kuu ya Tanzania mamlaka ya kusimamia uwekezaji unaofanywa na skimu za bima ya afya ya umma kwa lengo la kukuza mtaji na hivyo kuimarisha uhai na uendelevu. Vilevile, kifungu cha 30 kinaipa Mamlaka jukumu la kutoa miongozo kuhusiana na ukomo wa gharama za uendeshaji wa skimu ya bima ya afya ya umma ambapo dhumuni la kifungu hiki ni kuhakikisha skimu hizo zinakuwa na fedha za kutosha kujiendesha na kusimamia utekelezaji wa majukumu yake bila kuathiri utoaji wa huduma za bima ya afya.

Katika kuhakikisha kuwa haki za wanufaika na watoa huduma katika mfumo wa bima ya afya zinalindwa, kifungu cha 31 kinaweka utaratibu wa namna ambavyo Mamlaka itashughulikia malalamiko. Ili kuwezesha utekelezaji wa sharti la kujiunga na skimu za bima ya afya, Kifungu cha 32 kinaweka sharti la zuio la upatikanaji wa baadhi ya huduma za kijamii kama vile upatikanaji wa leseni ya udereva, bima za vyombo vya moto, kujiandikisha kidato cha tano na sita na vyuo, hati ya kusafiria, Viza, laini za simu na utambulisho wa Taifa. Kifungu cha 33 kinampa Waziri mamlaka ya kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa Sheria inayopendekezwa.

Kifungu cha 34 kinatoa katazo kwa wanufaika, vituo vya kutolea huduma za afya na skimu za bima ya afya kutoa taarifa za uongo na kuweka adhabu iwapo watathibitika kufanya hivyo. Dhumuni la kifungu hiki ni kulinda uhai na uendelevu wa skimu za bima ya afya na kuhakikisha huduma za bima ya afya zinatolewa na skimu zenye sifa. Vilevile, kifungu cha 36 kinatoa adhabu kwa mtu ambaye atakiuka masharti ya kifungu chochote cha Sheria hii. Dhumuni la kifungu hiki ni kuweka utaratibu wa kushughulikia makosa yote ambayo hayajawekewa adhabu mahsusi katika Sheria hii ili kuboresha uendeshaji wa mfumo wa bima ya afya kwa wote.

Kifungu cha 38 kinaweka ukuu wa Sheria inayopendekezwa katika masuala yanayohusu uendeshaji na usimamizi wa mfumo wa bima ya afya. Lengo la kifungu hiki ni kuondoa ukinzani wa sheria baina ya sheria hii na sheria nyingine yoyote inayohusiana na masuala ya bima ya afya.

Sehemu ya Nane inabainisha kufutwa kwa Sheria ya Mfuko wa Afya ya Jamii, Sura ya 409, na kuweka masharti ya mpito na yatokanayo. Kifungu cha 39 kinaeleza kuhusu kufutwa kwa Mfuko wa Afya ya Jamii. Dhumuni la kifungu hiki ni kubainisha masharti yatakayoendelea kutekelezwa ili kuhakikisha kuwa wanufaika wa Mfuko wa Afya ya Jamii wanaendelea kunufaika na mafao hayo hadi uanachama wake utakapo koma. Kifungu cha 40 kinaweka kipindi cha mpito kwa Mfuko wa afya ya Jamii kisichozidi miezi kumi na mbili tangu kuanza kutumika kwa Sheria inayopendekezwa. Hata hivyo, kifungu hicho kinampa mamlaka Waziri kuongeza kipindi cha ziada cha mpito kisichozidi miezi sita. Lengo ni kuhakikisha utekelezaji wa Sheria inayopendekezwa hausababishi malalamikokwa wananchi ambao tayari ni wanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii.

Sehemu ya Tisa inabainisha Sheria mbalimbali zinazopendekezwa kufanyiwa kutokana na Sheria inayopendekezwa kutungwa. Sheria hizo ni Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, Sura ya 395; Sheria ya Hifadhi ya Jamii, Sura ya 135; Sheria ya Bima, Sura ya 394; Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii, Sura ya 50; Sheria ya Paspoti na Hati za Kusafiria, Sura ya 42; Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438; Sheria ya Mtoto, Sura ya 13; Sheria ya Leseni za Biashara Na. 25 ya 1972; Sheria ya Usalama Barabarani; Sura ya 168; Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sura ya 366, Sheria ya Vyuo Vikuu, Sura ya 346 na Sheria ya Usajili na Utambauzi wa Watu, Sura ya 36. Lengo la marekebisho

ya Sheria hizo ni kuwezesha kufungamanisha huduma zitolewazo chini ya Sheria na wajibu wa kujiunga na skimu za bima ya afya.

Vilevile, Sehemu hii inapendekeza marekebisha ya Sheria Udhibiti wa Hospitali Binafsi, Sura ya 151 ili kuweka uwakilishi wa Mamlaka ya Bima katika bodi ya hospitali binafsi kwa lengo la kuboresha udhibiti wa hospitali hizo ambazo ni watoa huduma chini ya Sheria inayopendekezwa.

Dodoma,
29 Agosti, 2022

UMMY A. MWALIMU,
*Waziri wa Afya*